# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

## MKATABA WA KAZI YA UFUNDI WA KUTENGENEZA NA KUFITISHA MADIRISHA NA MILANGO YA GRILL UJENZI WA CHUO CHA VETA LUSHOTO

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 19 mwezi 05 2022

**KATI YA**

Mkurugenzi wa Kanda, **VETA Kanda ya Kaskazini, S.L.P. 1738, Moshi**, ambaye anaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802, Dodoma (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

**NA**

**MARK DISTRIBUTORS AND SUPPLIES CO. LTD** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundi") kwa upande mwingine.

**KWA KUWA** Mwajiri anajenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya LUSHOTO;

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya LUSHOTO;

**NA KWA KUWA** Mwajiri amempatia Fundi nakala ya michoro pamoja na mchanganuo wa kazi za Ujenzi vinavyoonyesha kazi zitakazofanyika.

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO;**

1. **GHARAMA YA UFUNDI**

   Kwamba, gharama za ufundi ni Shilingi za Tanzania 16,333,000.00 (Milioni Kumi na Sita laki tatu thelathini na tatu elfu tu.)

   Fundi atafanya kazi ya kutengeneza na kufitisha madirisha na milango ya grill kwa majengo kumi na tatu (13) kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

   Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

2. **MABADILIKO YA GHARAMA ZA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)**

Gharama ya Ufundi haitabalika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya Ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. **NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Malipo yatafanyika baada ya kupata hati ya uthibitisho wa kufanya malipo kutoka kwa Mhandisi msimamizi wa mradi na mwajiri atamlipa Fundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

(a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
(b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
(c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
(d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundi;
(e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi;na
(f) Baada ya kukamilika kwa"Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundi.

4. **MAKABIDHIANO YA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI**

a) Fundi atakabidhiwa kazi tarehe 20/05/2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote mbili zitaweka kumbukumbu ya maandishi siku ya makabidhiano na kusaini.

b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya **siku ishirini na moja** toka tarehe ya makabidhiano. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji inaweza kubadilika.

c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. **WAJIBU WA FUNDI**

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao:

a) kutengeneza na kufitisha madirisha na milango ya grill kwa majengo kumi na tatu (13) kama ilivyoainishwa kwenye mchanganuo wa kazi.

b) Kutekeleza maelekezo yote ya maandishi yanayotolewa na Mwajiri ndani ya muda utakaopangwa, iwapo Fundi hatatekeleza maelekezo yaliyotolewa ndani ya muda uliopangwa, Mwajiri anayo haki ya kumsimamisha Fundi kazi na kuajiri Fundi mpya ili atekeleze maelekezo hayo. Gharama za malipo za Fundi mpya zitatokana na sehemu ya fedha

aliyotakiwa kulipwa Fundi Mkuu kutokana na kazi husika aliyoshindwa kutekeleza.

c) Kumjulisha Mwajiri kwa maandishi kuhusu mapungufu yoyote atakayobaini katika michoro au mchanganuo wa kazi ili Mwajiri atoe maelekezo.

d) Kumjulisha Mwajiri anapokosa vifaa ili Mwajiri atoe maelekezo.

e) Kuwalipa watumishi au wasaidizi wake wanaomsaidia kutengeneza na kufitisha madirisha na milango ya grill kutokana na makubaliano yao.

f) Kuhakikisha usalama wa watumishi au wasaidizi wake, Mwajiri hatahusika na madai yoyote ya fidia yatakayotokea katika eneo la kazi.

g) Kuzingatia na kutekeleza masharti yote ya sheria za nchi zinazohusiana na kazi anayoifanya.

h) Kukubali kukatwa na Mwajiri kodi ya zuio (withholding tax).

i) Kurudisha kwa Mwajiri nyaraka na kumbukumbu zote zinazohusiana na kazi hii mara tu atakapomaliza kazi iliyoainishwa katika Mkataba huu.

## 6. WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri atakuwa na wajibu ufuatao:

a) Kumlipa Fundi malipo halali ya kazi iliyoainishwa katika Mkataba huu kulingana na utaratibu uliobainishwa katika kipengele na. 3.

b) Kutoa idhini ya kuanza kazi kutokana na ratiba ya kazi iliyowasilishwa na Fundi.

c) Kusimamia kwa ukamilifu kazi ya ufundi kama ilivyoainishwa katika Mkataba huu.

d) Kutoa maelekezo mbalimbali kwa Fundi wakati wa utekelezaji wa kazi.

e) Kuhifadhi michoro, mchanganuo wa vifaa pamoja na maelekezo yote ya maandishi yaliyotolewa na Mwajiri kwa Fundi.

f) Kuzingatia na kutekeleza masharti yote ya sheria za nchi zinazohusiana na kazi anayoifanya Fundi.

g) Kumkata Fundi kodi ya zuio (withholding tax).

7. **WATUMISHI WA FUNDI**

a) Fundi atatakiwa kuwa katika eneo la kazi muda wote anapotekeleza kazi yake. Hata hivyo, kipindi ambacho Fundi hatakuwa kwenye eneo la kazi kwasababu zilizoidhinishwa na Mwajiri, ataweka mtumishi wake ambaye ataendelea na usimamizi wa kazi kwa niaba yake.

b) Fundi ataweka utaratibu wake kwa ajili ya kupata watumishi wa kutosha watakaomsaidia kufanya kazi iliyoelekezwa katika Mkataba huu.

c) Mwajiri atakuwa na haki ya kumuagiza Fundi kumuondoa mtumishi wake ambaye atakuwa hafanyi kazi kama inavyotakiwa na Mwajiri kulingana na Mkataba huu.

8. **MSIMAMIZI WA KAZI**

a) Mwajiri atakuwa na haki ya kuweka Msimamizi wa kazi ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli kwa niaba ya Mwajiri. Fundi au Mwakilishi wa Fundi anatakiwa kutoa ushirikiano kwa Msimamizi wa kazi katika kutimiza majukumu yake.

b) Maelekezo yatakayotolewa kwa Fundi na Msimamizi wa kazi kwa maandishi kama ilivyoainishwa katika kifungu Na. 7(a), yatakuwa ni sawa na maelekezo aliyoyatoa Mwajiri kuhusu mambo yafuatayo:

i. Tafsiri ya maelekezo ya Mwajiri, michoro, maelezo na viwango, mchanganuo wa vifaa vya ujenzi.

ii. Uondoaji katika eneo la kazi vifaa ambavyo viko kinyume na Mkataba huu.

iii. Maelekezo ya uharaka yahusuyo usalama au ulinzi wa watu na mali.

iv. Maelekezo mengine ambayo Msimamizi wa kazi amepewa kwa maandishi na Mwajiri kuyasimamia.

c) Maelekezo mengine yoyote yatayotolewa na Msimamizi wa kazi ambayo hayako katika kifungu 8(b) cha Mkataba huu yatakuwa batili.

9. **KAZI ZINAZOFANYWA NA MWAJIRI AU MTU MWINGINE ALIYEAJIRIWA NA MWAJIRI**

Ikiwa taratibu za kazi zinaelekeza kuwa sehemu ya jengo linalojengwa na Fundi lifanywe na Mwajiri au mtu mwingine aliyeajiriwa na Mwajiri, Fundi atatakiwa kumruhusu Mwajiri au mtu mwingine aliyeajiriwa na Mwajiri afanye kazi hiyo.

## 10. MABADILIKO YA KAZI

a) Mwajiri anaweza kutoa maelekezo kwa Fundi akihitaji yafanyike mabadiliko ya kazi tofauti na michoro pamoja na mchanganuo wa vifaa. Mabadiliko yanaweza kuwa katika aina usanifu (design), ubora wa kazi (quality), kiasi cha kazi inayofanywa (quantity/extent of the works).

b) Mabadiliko ya kazi yanaweza yakapelekea kubadilika kwa gharama ya ufundi na pia kubadilika kwa muda wa kukamilisha ujenzi.

## 11. KUKAMILIKA KWA KAZI NA MUDA WA MATAZAMIO YA KAZI

a) Mwajiri atakapoona kuwa kazi imekamilika, atatoa kwa Fundi hati ya kukamilika kwa kazi. Kukamilika kwa kazi itakuwa ni ile siku iliyoandikwa katika hati ya kukamilika kazi.

b) Uharibifu wowote katika jengo utakaotokea ndani ya kipindi cha miezi sita tangu siku Mwajiri ametoa hati ya kukamilika kwa kazi, utarekebishwa na Fundi kwa gharama zake ndani ya siku thelathini tangu Mwajiri amjulishe Fundi juu ya uharibifu huo.

c) Mwajiri atakapoona Fundi amerekebisha uharibifu wote uliotokea ndani ya miezi sita, atatoa hati ya kukamilika kwa kazi. Kukamilika kwa kazi baada ya muda wa matazamio kutakuwa siku ile iliyoandikwa katika hati ya kukamilika kwa kazi baada ya muda wa matazamio.

## 12. FEDHA YA ZUIO

Kazi iliyoainishwa katika Mkataba huu ikikamilika, Mwajiri atabaki na 5% ya gharama ya kazi hadi pale muda wa matazamio ya kazi utakapokamilika. Fedha hizo zinaweza kutumika pale uharibifu unapotokea katika kipindi cha matazamio ya ujenzi na Fundi akashindwa au akakataa kurekebisha uharibifu huo ndani ya muda wa mwezi mmoja baada ya kupata maelekezo ya Mwajiri.

## 13. VITU VYA THAMANI VITAKAVOPATIKANA KATIKA ENEO LA KAZI

Vitu vyovyote vya thamani vitakavyoonekana katika eneo la kazi, Fundi atavitolea taarifa na vitakuwa mali ya Mwajiri.

## 14. MAMBO YALIYO NJE YA UWEZO WA KIBINADAMU

Itakapotokea jambo lolote lililo nje ya uwezo wa kibinadamu kama vile mafuriko, kimbunga, tetemeko la ardhi na mambo yanayofanana na hayo, pande zote mbili zitapata nafasi ya kulijadili na kulitafutia ufumbuzi wa haraka.

## 15. NOTISI (NOTICES)

Mawasiliano yote, Hati, Notisi yatakayofanyika katika Mkataba huu, yatafanyika kwa kupelekwa moja kwa moja (physically) kwa upande wowote wa Mkataba.

## 16. SHERIA ZINAZOTUMIKA

Sheria za kutafsiri Mkataba huu na ufanyaji wa kazi katika Mkataba huu ni sheria za Tanzania.

## 17. RUSHWA

Iwapo Fundi, watumishi au wasaidizi wake katika kutekeleza kazi hii watajihusisha na masuala yoyote ya rushwa ama jinai yoyote, basi Mwajiri anaweza kuvunja Mkataba huu.

## 18. KUVUNJWA KWA MKATABA

Mkataba huu unaweza kuvunjwa na upande wowote wa Mkataba huu.

(a) Mkataba kuvunjwa na Mwajiri:

Bila ya kuathiri haki zozote za Mwajiri, iwapo Fundi akifanya makosa yafuatayo:

i. Kutofanya kazi kwa siku tatu (3) bila ya sababu yoyote ya msingi, au

ii. Kutofuata maelekezo ya Mwajiri wakati wa kazi, au

iii. Fundi akimpa mtu mwingine kazi bila ya kupata idhini ya Mwajiri. Mwajiri atampa Fundi notisi ya siku saba ili arekebishe makosa hayo, iwapo Fundi hatarekebisha makosa hayo ndani ya muda huo, Mwajiri atavunja Mkataba huu na kudai kwa Fundi gharama zote ambazo zinaweza kuwa zimesababishwa na Fundi.

(b) Mkataba kuvunjwa na Fundi:

Bila ya kuathiri haki zozote za Fundi, iwapo Mwajiri akifanya makosa yafuatayo:

i. Mwajiri anasitisha kazi kwa zaidi ya kipindi cha siku kumi na nne, au

ii. Fundi asipopata maelekezo yanayohusu kazi kutoka kwa Mwajiri, michoro pamoja na makabrasha mengine anayopaswa kupewa na Mwajiri ndani ya siku saba baada ya muda ambao angepaswa kutoa maelekezo, michoro pamoja na makabrasha mengine, au

iii. Kuchelewesha vifaa (materials).

Katika mazingira hayo, Fundi atampa Mwajiri notisi ya siku saba (7) ili arekebishe makosa hayo, iwapo Mwajiri hatarekebisha makosa hayo ndani ya muda huo, Fundi atasitisha Mkataba huu na kudai kwa Mwajiri gharama zote ambazo zinaweza kuwa zimesababishwa na Mwajiri.

## 19. USIRI

Nyaraka zote zitakazokuwa zimetumika katika Mkataba huu hazitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa kazi zinazohusu Mkataba huu.

## 20. USULUHISHI WA MIGOGORO

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhisha mgogoro, basi upande wowote utatoa notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi (arbitration).

**IMESAINIWA NA KUWEKWA MUHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA MKURUGENZI WA KANDA, VETA KANDA YA KASKAZINI**

Jina: Funga D. R. Saini: [signature] MKUU WA CHUO CHUO CHA MKOA CHA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA

Wadhifa: MKUU WA CHUO Tarehe: 19/05/2022

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: FRANK R. KABIPE Saini: [signature]

Wadhifa: KATIBU KAMATI Tarehe: 19/05/2022

**IMESAINIWA NA FUNDI**

Jina: MARK DISTRIBUTORS & SUPPLIES CO. LTD Saini: [signature]

Wadhifa: FUNDI Tarehe: 19/05/2022

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: ANGEL EBEN Saini: [signature]

Wadhifa: SHAHIDI Tarehe: 19/05/2022